JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA WANGING'OMBE

Simu 1: 0262784505
Simu 2: 0262784507
Barua pepe:
md@ wangiwasa.go.tz
info@ wangiwasa.go.tz

Km 5 kutokaHalali,Njiapanda
Barabara ya Iringa-Mbeya
Mji Mdogo wa Ilembula
S.L.P. 317
**MAKAMBAKO**

# MKATABA WA KAZI YA UCHIMBAJI, ULAZAJI NA UFUKIAJI WA MABOMBA PAMOJA NA UFUNGAJI WA DIRA ZA MAJI

**MKATABA NO: .(AE/083/2021-2022/HQ/W/02 LOT 2)**

**MKATABA HUU** Unafanyika leo tarehe 22 Mwezi 11 Mwaka 2021

**BAINA YA**

**MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA WANGIN'GOMBE** wa S.L.P 317, **MAKAMBAKO** (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama **Mwajiri**) kwa upande mmoja wa mkataba.

**NA**

**ILEMBULA PLUMBING GROUP wa S.L.P**...31.....**ILEMBULA** (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama **Mwajiriwa**) kwa upande mmoja wa mkataba.

**KWAMBA**

Mwajiri anakusudia Mwajiriwa kufanya kazi ya Uchimbaji,Ulazaji na ufukiaji wa mabomba pamoja na ufungaji wa dira za maji eneo la Igwachanya kama ilivyoainishwa katika mkataba huu kifungu (i) 1 – 10 na kwamba mwajiriwa yupo tayari kufanya kazi hiyo kwa masharti ya mkataba huu.



22/11/2021

Scanned by CamScanner

**MKATABA HUU UNASHUHUDIA HAYA YAFUATAYO:**

## 1. MUDA WA KUANZA, UKOMO NA MAREKEBISHO.

i. Mkataba huu ni wa muda wa miezi minne (4) kuanzia tarehe ya kusainiwa kwa mkataba huu kwa kuzingatia programu ya kazi itakayotolewa na mwajiri.

ii. Pasipo kuathiri masharti ya kifungu namba moja hapo juu, katika kipindi cha utekelezaji wa mkataba huu, pande husika zinaweza kukutana na kukubaliana kufanya mabadiliko katika kifungu au vifungu vya mkataba huu kwa kadili itakavyoonekana inafaa.

## 2. WAJIBU WA MWAJIRIWA.

i. Mwajiriwa atahakikisha kazi anayoifanya inakuwa bora kwa viwango vinavyoelekezwa .

ii. Mwajiriwa atahakikisha anatekeleza kazi hiyo kwa muda uliokubalika kwenye mkataba.

iii. Mwajiriwa atahakikisha anakuwa na mafundi wake atakaokubaliana nao kumsaidia kazi yake kwa idadi itakayopelekea kufanya kazi hiyo kwa wakati uliokubalika.

## 3. GHARAMA ZA MKATABA NA UTARATIBU WA MALIPO.

i. Mwajiriwa atalipwa jumla ya kiasi cha Tsh 39,500,000.00 kama gharama ya kazi zote zilizoainishwa .

ii. Mwajiriwa anaweza kuomba sehemu ya fedha katika kazi ya ulazaji bomba na ufungaji dira za maji mara baada ya kukamilisha sehemu ya kazi na kufanyiwa tathimini na Mhandisi kiasi kinachostahili kulipwa ili kimwezeshe Mwajiriwa kuendelea kutekeleza majukumu yake.



22/11/2021

Scanned by CamScanner

iii. Fedha za Malipo ya kazi zitakazo kuwa zimefanyiwa tathmini na mhandisi zitalipwa na Mkurugenzi Mtendaji kwa mwajiriwa ndani ya siku kumi na nne (14) tangu tarehe ya kuwasilisha hati ya madai

## 4. MAJUKUMU YA MWAJIRI

i. Kusimamia kazi inayotekelezwa na mwajiriwa kwa kushirikisha kamati zilizoundwa na Mwajiri pamoja na wasaidizi wa mwajiriwa.

ii. Kuhakikisha Mwajiriwa analipwa kwa wakati fedha za kazi alizofanya kama ilivyobainishwa kwenye mkataba huu

iii. Kuhakikisha ubora wa kazi unafikiwa na kutoa maelekezo wakati wa ulazaji bomba na ufungaji dira za maji na huhakikisha maelekezo yaliyotolewa yanafanyiwa kazi.

iv. Kuhakikisha vifaa na mahitaji kwa ajili ya utekelezaji wa kazi yanapatikana (Kuwepo eneo la kazi) kwa wakati.

v. Kuhakikisha anatoa vifaa kwa Mwajiriwa kwa kutumia nyaraka maalumu (issue voucher) Mwajiriwa atakiri mapokezi ya vifaa hivyo kupitia nyaraka hiyo na msimamizi wa mwajiri atahakikisha mali hiyo (vifaa) vinatumika kwa uadilifu kama ilivyo kusudiwa.

vi. Atahakikisha usalama wa wafanyakazi na Mwajiriwa wa wasaidizi wa Mwajiriwa watakaokuwepo eneo la kazi na kuhakikisha huduma ya kwanza inakuwepo eneo la kazi ili kukabili dharura yoyote itakayojitokeza wakati wote wa utekelezaji wa kazi ikiwa ni pamoja na kuumia kazini.

## 5. MATUKIO YASIYOTARAJIWA ENEO LA KAZI

a. Tukio au jambo lolote litakalotokea wakati wa utekelezaji wa kazi ambalo halikutarajiwa na Mwajiri au Mwajiriwa na kama lipo nje ya uwezo wa pande zote mbili za mkataba huu na litakalopelekea kuchelewa kwa kazi matumizi ya muda wa ziada kwa kazi iliyokwama, majadiliano na makubaliano yatafanyika kati ya pande mbili za mkataba ili kufikia maamuzi ya tukio lililojitokeza ikiwa ni pamoja na utoaji wa ongezeko la muda la utekelezaji wa kazi ikibidi.



22/11/2021

Scanned by CamScanner

b. Endapo Mwajiriwa atasababisha hasara/kutokana na uzembe katika utekelezaji wa majukumu yake atawajibika kulipia fidia kwa hasara iliyojitokeza na pia hatua za kisheria zitachukuliwa kwa ziada ya hasara hiyo.

### 6. KUSITISHWA KWA MKATABA

a. Mwajiriwa atakuwa na haki ya kusitisha mkataba pale atakapoona au kuamini kwa namna yeyote ile Mwajiriwa atashindwa kukamilisha kazi ndani ya muda ulioainishwa kwenye mkataba huu, Mwajiriwa kushindwa kuendelea na kazi na Mwajiriwa kuonyesha udhaifu au uwezo mdogo wa kiufundi chini ya ule uliotarajiwa.

b. Mkataba huu unaweza kusitishwa na upande wowote wa mkataba huu kutoa taarifa ya maandishi ya siku nne (4) ya kusudio la kusitisha mkataba huu kama upande mwigine utashindwa kutekeleza mashariti ya mkataba huu.

### 7. SHERIA ITAKAYOTUMIKA

Mkataba huu utatafsiliwa kwa kutumia sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### 8. VIAMBATANISHO

Viambatanisho vifuatavyo vitasomwa pamoja na mkataba huu;-

i. Mchanganuo wa bei (BOQ)
ii. Leseni ya biashara
iii. Katiba ya kikundi

### 9. UTATUZI WA MIGOGORO

Kwamba iwapo utatokea mgogoro wowote ule kutokana na mkataba huu utatatuliwa kwanza nje ya mahakama na msuluhishi ambaye atakuwa ni katibu Tawala wa Wilaya ya Wangin'gombe.



22/11/2021

Scanned by CamScanner

**KWA USHUHUDA HUU**, pande zote mbili zinaweka saini zao katika mkataba huu siku na tarehe kama ilivyo hapa chini:

**1. KWA NIABA YA MAMLAKA YA MAJI:**

Jina MUSSA D. MASASI

Cheo MKURUGENZI MTENDAJI

Sahihi [signature]

Tarehe 22/11/2021

MKURUGENZI MTENDAJI MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA WANGING'OMBE

**MWAJIRIWA**

Jina CLEMENT E. KAYEGA

Cheo MWENYEKITI

Sahihi [signature]

Tarehe 22/11/2021

ILEMBULA PLUMBING GROUP S.L.P. 31 ILEMBULA

**SHAHIDI WA MAMLAKA YA MAJI**

Jina WILFRED M. GICHOGO

Cheo MENEJA UFUNDI

Sahihi [signature]

**SHAHIDI WA MWAJIRIWA**

Jina ASANTE X. SANGA

Cheo KATIBU

Sahihi [signature]

[signature]

TWANUSITILE SIMANYANI
ADVOCATE
22nd NOV 2021

TWANUSITILE CHARLES SIMANYANI ADVOCATE NOTARY PUBLIC & COMMISSIONER FOR OATHS P.O. BOX 102, MAKAMBAKO



Scanned by CamScanner